102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
(Lugha)
Juni 2010
Saa: 2 ½

Maagizo

a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Weka sahihi yako na darasa lako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
c) Jibu maswali yote
d) Ni lazima watahiniwa waangalie kama kurasa zote zimepigwa chapa sawawa na kuwa maswali yote yamo
e) Andika majibu yako katika nafasi ulioachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Wakati dunia ikiwa inapambana na virusi vya ukimwi (VVU), aina nyingine ya virusi inaonekana kupata umaarufu kwa watumiaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Inaelezwa kuwa virusi vya kompyuta (VVK)vimetengenezwa kwa makusudi tofauti na vile vya ukumwi ambavyo vimekuwa ni suala tete, kwani wengine wanadai vimeandaliwa na wanasayansi katika maabara huko Los Angels, Marekani. Pia wapo wanaodai kuwa virusi vya ukimwi vimetokana na uhusiano wa binadamu na sokwe wa misitu ya Afrika ya Kati. Kati ya hao waliodai VVU vilitengenezwa, waligawanyika katika dhana mbili kuhusiana na kusudio lao. Dhana ya kwanza inaelezwa ilikuwa ni bahati mbaya, yaani maradhi, walipata matokeo ambayo hawakuyakusudia na pia wakashindwa kuyadhibiti. Wengine wanadai kwamba VVU vilitengenezwa kwa makusudi na nchi zilizoendelea kwa minajili ya kupunguza idadi ya watu katika nchi za dunia ya tatu, hasa zilizo Kusini mwa jangwa la Sahara, ambalo ndilo lililo na robo tatu ya waathirika wa ukimwi, kwa mujibu wa shirika la Afya Duniani (WHO).

Wakati virusi vya ukimwi vikishambulia binadamu, vya kompyuta hushambulia kumbukumbu zinazohifadhiwa kwenye kompyuta. Konpyuta ni chombo kinachotumika kurahisisha ufanisi wa kazi, ambapo kwa sasa zipo katika kila ofisi iwe ya serikali, taasisi au watu binafsi. Virusi vinavyoshambulia kazi katika kompyuta vimekuwa gumzo katika kila sehemu ambako teknolojia hii hutumika, na kuwa kikwazo katika ufanisi wa kazi unaotumia teknolojia mpya ya habari na mawasiliano (teknohama), hasa matumizi ya kumpyuta.

Awali kompyuta zilionekana kama adui mkubwa kwa ajira, kwani kazi ambazo hufanywa na watu kumi, huweza kufanywa na mtu mmoja kwa kutumia teknolojia hiyo, hivyo kuchukiwa sana na wafanyakazi kama ilivyokuwa kwa Waingereza walioandamana, kufanya vurugu na kuziharibu mashine zilizogunduliwa kurahisisha kazi katika kiwanda cha nguo mwaka 1811. Vurugu hizo zilifahamika kama 'Luddism'. Hapo nchini, tulizipokea kompyuta kwa kuzivumilia na kuziamini katika ufanisi wa kazi mbalimbali ikiwa ni kukubaliana na mapinduzi ya tasnia ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Mwaka 2000 baada ya Watanzania kujua umuhimu wa kompyuta, soko la kompyuta na vifaa vyake limekuwa likiongezeka kila siku. Kwa asilimia kubwa watumiaji wakubwa wa kompyuta hapa nchini ni vijana ambao wamepata mafunzo ya teknolojia hiyo shuleni na vyuoni.

Wengine hudiriki kusema kuwa hizi ni 'zama za vijana' kwa kuwa vijana ndio wanatumia sana kompyuta. Huwezi kuvuka barabara au mitaa zaidi ya miwili jijini Dares Salaam, hasa Kariakoo na Posta bila kuona duka linalouza kompyuta zilizotumika (mitumba) na vifaa vyake kutoka Ulaya na Marekani, ambazo huuzwa kwa bei nafuu na hunuliwa zaidi kuliko mpya.

Huenda ni katika utekelezaji wa sera ya soko huria na utandawai, achana na zile zilizo mpya kabisa. Kwa kuwa bidhaa za mitumba ni mchakato mzuri kuelekea katika jamii yenye kuhabarika, lakini shida kubwa ipo kwenya hivi virusi vilivyotengenezwa kwa makusudi na kushambulia kumbukumbu katika kompyuta.

Dhamira ya kutengenezwa virusi hivi haijaweza kufahamika sawasawa, lakini kwa kuwa ni wafanyabiashara bila shaka vilitokana na wazo la kibiashara la hao watengenezaji wa kompyuta. Kompyuta iliyovamiwa na virusi hupoteza baadhi ya nyaraka zilizohifadhiwa katika vifaa vitumikavyo kubebea nyaraka hizo kutoka kompyta moja hadi nyingine. Mara kadhaa kompyuta iliyoathirika kutokana na virusi hivi vinakosesha furaha ya kutumia kompyuta kwa kuwa kazi zinazohifadhiwa kielektroniki zinatishiwa usalama na virusi. Huenda baadhi ya watu wanaosema virusi vya kompyuta vimetengenezwa kibiashara wako sahihi, kwa kuwa kuna kinga dhidi ya virusi hivyo hatari. Kinga hiyo huuzwa kwa ajili ya kuingizwa katika kompyuta ili kusaidia ulinzi.

Mmoja wa wajasiriamali wa huduma za intaneti katikati ya jiji la Dar es salaam, ambaye ni mtaalamu wa taaluma ya teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) anasema: “Inakera sana na mimegundua kuwa ofisi nyingi za serikali hazifanyi baadhi ya kazi za uhazili ofisini mwao kwa kuhofia kupoteza nyaraka muhimu, hivyo kwenda katika steshenari za mitaani zilizo karibu nazo kwa kuhudumiwa. “Lakini kutokana na kupokea kazi mbalimbali kutoka sehemu zisizo na uhakika wa usalama, steshenari hizo huathiriwa na mara nyingine kompyuta zao kuharibika.”

Maswali

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)
_____

b) Fafanua chimbuko la virusi vya ukimwi kulingana na taarifa. (alama 2)
_____
_____
_____
_____

c) Ni nini tofauti kati ya virusi vya kompyuta na vile vya ukimwi kulingana na taarifa? (alama 2)
_____
_____
_____
_____
_____

d) Kwa nini wafanyakazi walikuwa na maoni hasi kuhusu kompyuta? (alama 2)
_____
_____
_____
_____
_____

e) Mwandishi anadai kuwa bidhaa za mitumba za kompyta ni duni. Fafanua. (alama 2)
_____
_____

f) Eleza lengo la kutengeneza virusi vya kompyta. (alama 2)

_____
_____
_____
_____
_____

g) Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumika katika ufahamu (Alama 4)

i) Wajasirimali

_____
_____
_____

ii) Virusi vya kompyuta

_____
_____
_____

iii) Soko huria

_____
_____
_____

iv) Utandawazi

_____
_____
_____

2. **UFUPISHO**

Tukichungua maisha ya vijana wa leo kwa jicho la kuona ndani sana, tutavumbua mambao mengi ya kushtusha. Lengo kuu la vijana hawa ni kupata kazi zenye chungu ya pesa, nyumba nzuri, tofauti na za kiafrika, magari mazuri yenye nguvu na mbio na mitambo mingine yenye kuwawezesha kutenda mambo bila ya kukipurikisha kiungo chochote. Wao wataka shida ziwe ng'ambo ya uoni wao.

Mapenzi, yaliyoitwa umoja wa masikilizano ya kinyumba na kilimwengu sasa yamegeuzwa na vijana wa leo yaitwe uhayawani, dosari, kutosikilizana na ari ya kujiokoa nafsi zao zinazoteketea. Mara nyingine watoto wa kike waolewapo na iwapo wanafanya kazi kama mabwana zao, hao huwa kwa thuluthi kubwa ya maisha yao, wanajitegemea na kujiona kama wanaishi na mabwana zao kama ada tu, bali wana uhuru wa kutenda vyovyote vile wapendavyo.

Iwapo wake wa namna hii watakemewa, hutisha kuwa watawaacha mabwana au kila mmoja wao awe na sehemu ya utawala katika nyumba zao maana kila mmoja anacho mwenziwe alichonacho. Bwana ana pesa – bibi anazo, bwana ana gari – bibi analo, bwana ana digrii- bibi anazo nyingi na kadhalika.

Vijana wa kiume wawapo hawana ari ya kuoa, wazazi wengi wana wa kike hupata hasara kubwa kama mfalme kuondolewa jeshi lake la adui wake: wasichana walioachiwa kazi mahsusi kuzitenda au wasichana shuleni, waingiapo katika zogo na zahama za vijana waleo za masinema, magoma ya mchana na usiku na mikutano isiyokwisha mara hushtukia wameingia katitka njia ya umama na mababa hawajulikani. Iwapo baba anajulikana, thuluthi tisaini na tisa kwa mia ya wazazi wa namna hii, hukataa katakata kuwa wahusika wa mambo za namna hii.

Yote haya yanasababishwa na mtambo mkubwa wa uhalifu-pesa. Wanawali wengi hutoa jasho kwa kufukuza pesa wazionazo upeoni mwa macho yao. Wasichana hawa huwaghilibu wavulana ambao wamezikokota katika matope.

Vijana wengine huwa radhi kabisa kupoteza maisha kwa kuingilia uhalifu ili wapate uti wa kuwawezesha kustarehe na wasichana na majumba yauziwayo pombe na wale wanyonyaji wazururao katika barabara pana za miji mikubwa nchini ya taa zenye rangi. Wasichana hujiharibu wajihi wao wakawa kama vyinyago vya uzazi wa kale.

MASWALI

a) Kulingana na aya tatu za kwanza, vijana wa siku hizi hupendelea kuishi maisha ya aina gani? (alma 7) (Utiririko al. 1) (Maneno 70-80)

Nakala chafu

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

Jibu

b) Maisha ya vijana yana madhara gani kwa vijana wasipokuwa na tahadhari ya maisha? (alama 6) (Utiririko-al. 1) (maneno 60-70)

Matayarisho

Jibu

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

a) Taja sauti iliyo na sifa zifuatazo. (alama 1)
i) Mbele ii) Tandazwa iii) Wastani

b) Weka shada katika neno lifuatalo kisha ueleze maana mbalimbali zinazojitokeza. (alama 2)
Ala

c) Ainisha mofimu katika neno: (Alama 2)
Achanikaye

d) Yakinisha sentensi ifuatayo kwa ukubwa: (alama 2)
Jibu la kitaalamu katika jitabu hili la ulimaji limewafanya wakulima wajinufaishe kutokana na mazao mazuri mashambani mwao.

f) Tumia neno ‘shamba’ kama nomino na chagizo ya namna mfanano katika sentensi moja. (alama 2)

g) Tumia jozi ya maneno yafuatayo kutunga sentensi moja. (alama 2)
Tekeleza na telekeza

h) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika tungo hili. (alama 2)
Tumetengeneza barabara.

i) Tunga sentensi yenye mpangilio wa vipengele vifuatavyo: (Alama 4)
i) Nomino ya kawaida
ii) Kivumishi cha sifa
iii) Kielezi cha namna halisi
iv) Kitenzi halisi
v) Kihusishi cha mahali
vi) Nomino ya kawaida

vii) Kivumishi cha sifa
viii) Kielezi

j) Akifisha :
Andua mtoto wa Chendeke alingolewa meno na askari
Atega alishangaa

k) Onyesha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo: (alama 3)
Wengi waliokewa mikate kwa tanuri na mpishi. (alama 2)

I) Ainisha vishazi katika sentensi hii. (alama 2)
Mwanafunzi aliyesoma kwa bidii amefuzu mtihani wake.

m) Ainisha virai katika sentensi hii. (Alama 2)
Lunalo aliikata miti yote iliyokuwa kando ya barabara kwa panga.

n) Tumia mistari kuchanganua sentensi ifuatayo. (alama 4)
Uchanganuzi unaowatatiza wanafunzi wengi ni ule unaohusu matawi

o) Badilisha kitenzi 'kuleta' kiwe katika hali ya kuamuru kisha utungie sentensi. (alama 2)

p) Fafanua matumizi ya 'jinsi' katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Wanyama jinsi hii wanastahili kufugwa.

q) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi wa taarifa. (alama 2)
« Kesho ninataka nyote mje na majembe! » Alisema Chifu wa kata yetu.

"Itabidi tuipalilie miti yote kdwani imeanza kuharibiwa na magugu.

r) Andika katika kinyume: (alama 2)
Zilizala ilipotokea wanafunzi walibabaika na kuanza kulia

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

1. a) Eleza maana ya:
i) Sajili (alama 1)
ii) Pijini (alama 1)

b) Huku ukitoa mifano, fafanua changamato zinazoikabili Kiswahili kama lugha ya taifa. (alama 4)

Soma kifungu kifuatacho kisha jujibu maswali yanayofuata

MTU I: Nikuuzie nini leo? Kuna nguo nyingi za kisasa na viatu..

MTU II: (akiangaza kote kote) ah! Sijui kama nitaweza kuinunua nguo niliyokuwa
Nikiitamani. Hii hapa. Ni kama imekuwa *so expensive*.
Juzi ulikuwa waiuza kwa bei afadhali.

MTU I: Kwani una *how much*? Hata hujasema ulicho nacho tuone kama nitaweza kukuuzia.

MTU: II (Mikono mifukoni) Naona kama sitaweza kwa kuwa waiuza shilingi elfu na mia tano hali mimi nina mia tisa tu!

MTU I: *(Anaibinya midomo kabla ya kuendelea kuongea)*. Hat mia tisa ni pesa ila hata mimi sijaipata kwa pesa hizo. Ongeza zifike angaa elfu na mia nne. Mia ni *discount* nzuri. Hiyo ni bei *poa.*

MTU II: Bado *hujareduce* chochote. Nami basi nimekuongezea mia. Elfu nzima ni pesa nyingi! Hata nitabaki bila nauli. Lakini maadamu nimepata nguo si hoja, naweza kutembea hadi nyumbani.

MTU I: (Kwa dhati) Hiyo ni bei ya *whole sale*. Labda uwe wanunua nguo kadah . *Otherwise* bei hiyo haifai kwa nguo moja tu. Wataka ngapi?

MTU II: *I wish* ningekuwa na…

c) Hii ni rejista gani? (alama 1)

d) Kwa kutolea mifano mwafaka, fafanua sifa tatu za rejista hii. (alama 3)